

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Tanga
01 Machi, 2025

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewahakikisha wawekezaji kuwa "Tanzania imefunguka kwa uwekezaji, Tanzania ni salama kwa uwekezaji, na sera za uwekezaji za Tanzania ni rafiki na endelevu."

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema kuwa Serikali inazidi kuwakaribisha wawekezaji na kuwa itaendelea kuweka sera rafiki, zinazotabirika na zinazowazesha wawekezaji nchini kuwa washindani katika soko la ndani na soko la kimataifa.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo wakati akiweka jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Kala wa kuhifadhia gesi ya LPG ya GBP Tanzania katika Jiji la Tanga. Uwekezaji huo unaogharimu dola za marekani milioni 50 unaendana na lengo la Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia la kuimarishe upatikanaji wa gesi ya kupikia.

Rais Dkt. Samia amesema kuwasikia na kuwaona wawekezaji mbalimbali ikiwemo kampuni ya GBP wakieleza kuwa wananzaika na mazingira bora ya uwekezaji nchini ni kielelezo kuwa sera za biashara na uwekezaji zinaleta matokeo yanayokusudiwa.

Katika hatua nyingine Rais Dkt. Samia amefanya ziara katika Bandari ya Tanga kujionea maboresho yaliyofanywa na Serikali kuitia uwekezaji wa Shilingi Bilioni 429 uliomarisha uwezo na ufanisi wa bandari hiyo.

Akizungumza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Rais Dkt. Samia amesema kuwa maboresho yanayofanywa na Serikali katika Bandari Kuu kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi, yaani Dar es Salaam, Mtwara na Tanga kwa sasa na Bagamoyo kwa siku zijazo, yanaenda kuihakikisha Tanzania nafasi yake kama lango kuu



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



la kuingia Afrika Mashariki na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara, viwanda na uwekezaji.

Akizungumzia uimarishaji wa miundombinu katika Mkoa wa Tanga, Rais Dkt. Samia amesema kuwa Serikali imepanga kujenga Barabara ya Handeni-Kiberashi-Kijungu hadi Singida kwa utaratibu wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP).

Rais Dkt. Samia amesema barabara hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya Bandari ya Tanga, na Serikali itamtafuta mwekezaji atakayejenga barabara hiyo kwa fedha zake mwenyewe na kisha watumiaji ikiwemo malori ya mizigo kulipia matumizi ya barabara hiyo inayofupisha safari.

Leo Rais Dkt. Samia amehitimisha ziara yake ya siku 7 mkoani Tanga ambapo alifika katika Wilaya zote 8 za Mkoa wa Tanga ambapo alizungumza na wananchi na kutembelea miradi ya maendeleo ya Serikali yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 600 na miradi ya sekta binafsi yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 500.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Sharifa B. Nyanga".

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

